


UTANGULIZI

Pangani ni wilaya mojawapo ya wilaya zinazounda mkoa wa Tanga. Wilaya hii ilianzishwa enzi za ukolononi na ni mojawapo ya wilaya za zamani sana hapa nchini.

Kijiografia Wilaya hii inapakana na wilaya ya Bagamoyo (ambayo ipo mkoa wa Pwani) upande wa kusini, upande wa magharibi imepakana na wilaya ya Handeni, upande wa mashariki imezungukwa na Bahari ya Hindi na kwa upande wa Kaskazini imepakana na wilaya muheza.

Wilaya ya Pangani ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 1830.8. Kutokana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, wilaya ya Pangani ina jumla ya watu 54,025 kati yao wanaume ni 26,870 na wanawake ni 27,155.



DIRA, DHIMA NA MALENGO

DIRA

“Jamii yenye maisha bora iliyohamasika, inayoendana na mabadiliko na iliyoendelevu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ifikapo 2016”

DHIMA


“Kutoa huduma bora kwa ufanisi na uhakika, uwezo na utawala bora katika kuinua maisha ya jamii yetu huku ikitunza utamaduni wake na urithi wa asili”

MALENGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI

1. Huduma ya Ukimwi kuboreshwa na maambukizi mapya kupunguzwa.
2. Kupiga vita na kudhibiti Rushwa.
3. Ubora wa kiwango cha huduma za kiuchumi na miundombinu kuongezeka.
4. Demokrasia, ushiriki wa jamii na utawala bora kuimarishwa.

5. Matumizi ya ardhi endelevu, ubora na upatikanaji wa huduma za ugani kuongezeka
6. Maliasili, utunzaji wa mazingira uwezo wa wanawake kuimarishwa.
7. Usawa wa kijinsia na ujengaji uwezo wa wanawake kuimarishwa
8. Kuwa tayari kukabaliana na majanga na mabadiliko ya hali ya hewa kuimarishwa
9. Kuwa na vyanzo vya mapato vyenye tija kupitia fursa mbalimbali za uwekezaji.

SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA WILAYA YA PANGANI

| SEKTA | PICHA ZA SHUGHULI ZA SEKTA HUSIKA |
|-------|--|
| Uvuvi |  <p>Kilimo cha zao la Mwani- Pangani</p>   <p>Uvuvi wa samaki -Pangani</p>  |

Boti zinazotomika katika shughuli za Uvuvi- Pangani



Picha ya juu ya Mto Pangani

Utalii



Picha ya Fukwe nzuri, safi na Pana zinazopatikana Pangani







Mandhari nzuri ya Bahari ya pangani huvutia sana watalii



Majengo ya kale, ya enzi ya mkoloni- jingo hili ni Bandari



Wanyama wakivinjari katika mbuga ya Saadani- ambayo

| ipo Pangani | |
|---------------------------------|--|
| <p>Kilimo na ufugaji</p> | <p>d</p>  <p>kilimo cha umwagiliaji, ndani ya wilaya ya Pangani</p>  |
| |   <p>Popoo (betel Nut) Zao la kipekee linalolimwa –Pangani Kijiji cha Mseko, Mauya na Kigurusimba</p> |

WAJIBU WA TAASISI

Halmashauri ya wilaya ya Pangani ina wajibu wa kuhakikisha huduma za kijamii zinazotolewa katika ngazi zote ni bora na zenye kukidhi mahitaji katika makundi yote ya jamii. Hivyo Halmashauri inawajibika kufanya yafuatayo:

1. Kuhakikisha huduma zitolewazo zinakidhi matarajio ya wananchi
2. Kuhakikisha huduma zinazotolewa ni sahihi, bora na kwa muda muafaka.
3. Kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma sawa bila ya kuangalia itikadi, dini, wala kabila
4. Kuhakikisha huduma inatolewa kwa uwazi.
5. Kuhakikisha mapato yanayopatikana yanatumika kwa kutoa huduma stahiki kwa jamii.
6. Kuimarisha ushirikiano mzuri na taasisi zingine zinazotoa huduma muhimu katika jamii.

JINSI YA KUFIKA PANGANI

Pangani inafikika kwa usafiri wa Barabara, usafiri wa anga na Usafiri wa majini

Usafiri wa barabara- Barabara ya Tanga jiji -Pangani, Barabara ya Muheza –Pangani Barabara ya Bagamoyo kutokea mkoa wa Dar es salaam, Pwani hadi Pangani Barabara zote zinapitika vizuri

Usafiri wa Anga- Wilaya ya pangani ina viwanja viwili vya ndege, Kiwanja cha ndege cha Mashado na kiwanja cha ndege kidogo cha Ushongo.

Usafiri wa majini

Wilaya ya Pangani inafikika kwa usafiri wa majini pia, kupitia bahari ya Hindi kwenda Zanzibar, Mombasa, Dar es Salaam, Tanga hadi pangani.

HITIMISHO

Kutokana na kuthamini wateja wetu kwa kutoa huduma za kijamii zilizo bora, wilaya ya Pangani inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kuunga mkono juhudi zetu za kutoa huduma kwa jamii yote kwa haki na usawa na kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI



MAWASILIANO

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA YA PANGANI

S.L.P 89, PANGANI- TANGA

SIMU: +255 (0) 27 2630058

NUKUSHI: +255 (0) 27 2630058

BARUA PEPE: ded@panganidc.go.tz